**Maswali na Majibu**

1. Waisraeli walihitajika wafanye nini siku ya 14 kwa mwezi wa kwanza?
   *Wachinje mwana kondoo wa kiume bila kuvunja mfupa na wamwoke*.
2. Yule mwana kondoo aliyeokwa walimkula na nini?
   *Mkate usiotiwa chachu na mboga chungu*
3. Walifanyia nini damu ya mwana kondoo?
   *Walipaka kwa miimo ya milango na juu vizingitini*.
4. Nini ilifanyika usiku wa manane?
   *Malaika wa kifo aliua wazaliwa wa kwanza wa Misri.*
5. Nyumba gani ndizo malaika wa kifo aliruka bila kuingia na asiue mzaliwa wa kwanza?
   *Nyumba za Waisraeli penye walikuwa wamepaka damu kwa milango.*
6. Waisraeli walinaswa namna gani kando ya Bahari ya Shamu?
   *Farao na jeshi lake walikuwa nyuma yao. Bahari ilikuwa mbele.*
7. Walivuka Bahari ya Shamu namna gani?
   *Musa alinyosha fimbo yake juu ya bahari na Mungu akaleta upepo wa nguvu uliosukuma maji kando na njia kavu ikawa katikati ya bahari.*
8. Chakula gani chenye Waisraeli wamekula tangu wakati ule?
   *Chakula cha Pasaka wakikumbuka vile Mungu aliwaokoa Misri.*
9. Tunakula nini kwa kila juma na huwa tunakumbuka nini?
   *Mkate na divai na tunakumbuka vile Yesu alituokoa kutoka kwa dhambi na kifo.*
10. Waisraeli walibeba nini kutoka kwa nchi ya Misri wakienda nchi ya ahadi?
    *Mifupa ya Yusufu.*

## Mistari ya kukariri

Kutoka 12:13; Kutoka 13:14; Waebrania 11:28 – 29; Yohana 1:29

## Mazungumzo

Soma 1 Wakorintho 5:7 na Yohana 1:29. Zungumza vile Yesu ni Mwana Kondoo wa Mungu na Yeye ndiye Mwana Kondoo wa Pasaka. Nini inaonyesha kwamba Waisraeli kuokoka kule Misri na vile Wakristo wanaokolewa na Yesu iko sawa.

## Kuandika

Jifanye Kwamba wewe ni Mwisraeli umepiga kambi karibu na Bahari ya Shamu.
Eleza vile ulinaswa wakati Magari ya jeshi la Misri lilikuwa likija. Andika vile ulivuka Bahari ya Shamu na ukaokoka kutoka kwa Wamisri.

# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

## Somo la 13 Pasaka

**SOMA Kutoka 12:1 – 42; 14:5 – 31**

**SOMO**

Baada ya kuwa na tauni tisa kule Misri, Mungu aliambia Musa na Haruni kwamba Waisraeli wanatakiwa wawe tayari kuotoka Misri. Mungu alipea Musa maagizo yasiyokuwa ya kawaida yenye walitakiwa watii kikamilivu. Siku ya 14 ya mwezi wa kwanza kila familia itachinja mwana kondoo mume na wamwoke. Na wawe waangalifu wasivunje mfupa wa yule mwana kondoo. Hiki kitakuwa chakula cha mwisho wao kukula wakiwa Misri. Watakula yule kondoo jioni. Watamkula na mkate usiotiwa chachu (mkate laini wa mfiringo uliookwa bila chachu) na mboga chungu. Watakula hicho chakula kama wamesimama na wawe wamepanga vyombo vyao tena wamevaa tayari kuondoka.



Mungu aliamrisha kwamba kabla hawajakula hicho chakula lazima wachukuwe damu ya mwana kondoo na wapake kwa miimo na vizingiti vya juu ya milango ya nyumba zao. Lakini wabaki ndani ya nyumba zao ili waokoke.

Mungu alisema usiku huo, watoto wa kwanza katika kila nyumba ya Wamisri watauwa. Usiku wa manane ulipofika Mungu alituma malaika wa kifo kuwauwa wana wote wa kwanza katika kila nyumba ya Wamisri. Lakini malaika wa Mungu alipita kila nyumba iliyokuwa ya Waisiraeli kwa sababu ilikuwa imepakwa damu kwenye milango. Kila mmoja aliyekuwa kwenye nyumba iliyopakwa damu alibaki akiwa salama.

Baada ya tauni mbaya hii, Farao alisoma somo. Alisema kwamba Waisraeli wanasitahili kuondoka. Wamisri walifadhaika sana na wakawaomba Waisraelii waondoke. Waliwapa fedha, dhahabu na vitu vingine vya dhamani na kuwaambia waondoke. Mwishowe Waisraeli waliondoka Misri. Wakawa huru kutoka utumwani.

Taifa kubwa la Israeli lilitoka Misri na mifugo wao na mali yao yote. Walisafiri kuelekea mashariki mpaka wakafika kwa Bahari ya Shamu. Punde si punde walisikia nyuma yao vishindo vya farasi. Farao alikuwa amebadilisha mawazo yake na alitaka arudishe Waisraeli utumwani kule Misri.

Waisraeli walinaswa. Jeshi la Misri lilikuwa nyuma yao na Bahari ya Shamu mbele yao. Lakini Musa aliwapa moyo akawambia, "Kaa kimya na mtaona vile Mungu atawaokoa." Musa alinyosha fimbo yake kwenye bahari na Mungu akaleta upepo wa nguvu ukavuma usiku kucha. Upepo uligawanyisha maji na kukawa na njia katikati ya bahari. Kulipofika asubuhi, Waisraeli walitembea katikati ya bahari kwa njia kavu. Jeshi la Wamisri waliwafwata. Wakati Waisraeli walipofika n'gambo, Musa alinyosha ile fimbo tena juu ya bahari. Mawimbi ya bahari ilirudi kwa kasi na kufunika Farao na jeshi lake na kuwaangamiza.

Mungu aliokoa Musa na Waisraeli kutoka kwa Farao. Walishukuru Mungu na kumsifu. Halafu walianza safari ya kuenda kwa nchi yenye Mungu aliwaahidi.

Mungu aliambia Waisraeli kwamba kila mwaka wanatakiwa wakumbuke vile Mungu aliwaokoa kutoka kwa Wamisri. Kutoka wakati huo, Waisraeli huwa wanakumbuka vile Mungu aliwaokoa kwa njia ya maajabu kutoka Misri. Wanakula chakula kama vile Waisraeli walivyokula usiku wao wa mwisho kule Misri. Wanakula mwana kondoo aliyeokwa, mkate usio na chachu na mboga chungu. Wanaita hiki chakula 'Pasaka', Kwa sababu Mungu aliwaokoa wakati malaika wa kifo alipokuwa akiruka nyumba zao. Mwanao mdogo katika familia akiuliza,"Mbona tunafanya hivyo?" Baba atamwambia hadithi ya Pasaka ya kwanza na vile Mungu aliwaokoa kutoka Misri. Wakati huu, hawa watu wa Mungu wanaitwa 'Wayahudi'. Bado wanatimiza hiki chakula cha Pasaka na kukumbuka vile Mungu aliwaokoa watu wake.

Mungu alikuwa amewaahidi kwamba atawatoa kutoka Misri na kuwaongoza mpaka nchi aliyowaahidi. Mungu aliokoa Waisraeli watu wake. Mungu aliwaokoa kutoka kwa malaika wa kifo baada ya wao kuua mwana kondoo na kupaka damu kwa milango yao. Tena Mungu aliwaokoa kutoka kwa jeshi la Misri alipowatengenezea njia katikati ya Bahari ya Shamu.

Musa na Waisraeli waliokoka kutoka Misri kwa sababu walifanya vile Mungu alikuwa amewaambia. Waliamini kwa ahadi za Mungu na kutii neno lake. Waisraeli waliamini Mungu - walikuwa na imani. Soma Waebrania 11:28 – 29. **Tunaweza** kuokoka kutoka kwa dhambi na kifo **tukiwa** na imani.

Kuna mambo yaliyokuwa yakifanyika kwa Agano la Kale yanakuwa kama picha yakionekana kwa sababu ya Mungu baadaye. Haya mambo yana mafunzo kwetu. Hasa kisa cha Waisraeli kuokoka kutoka Misri inalinganishwa na sisi kuokoka kutoka kwa dhambi kupitia kwa ubatizo na tuwe Wakristo.

| Waisraeli | Sisi |
|---|---|
| Mungu aliahidi kuwapeleka Waisraeli kwa nchi ya ahadi. | Mungu aliahidi kwamba atatuma Yesu kusimamisha Ufalme hapa duniani. |
| Waisraeli waliua mwana kondoo. Damu ya Mwana kondoo ilipakwa ili iwaokoe kutoka kifo. | Yesu ni mwana kondoo wa Pasaka. Alikufa. Damu yake ilimwagika ili ituokoe kutoka kwa dhambi na kifo. |
| Mifupa ya mwana kondoo haikuvunjwa. | Mifupa ya Yesu haikuvunjwa. |
| Waisraeli walienda katikati ya maji ya Bahari ya Shamu. | Sisi tunaenda kwa maji ya ubatizo. |
| Mungu aliwapitishia Waisraeli jangwani akiwapeleka kwa Nchi ya ahadi. | Mungu ako nasi kwa maisha ya saa hii anatuelegeza kwa Ufalme. |
| Waisraeli wanatimiza chakula cha Pasaka kila mwaka wakikumbuka vile Mungu aliwaokoa kutoka Misri. | Tunavuna mkate na kuinywa divai tukikumbuka vile Yesu alituokoa kutoka kwa dhambi na kifo. |

Waisraeli walichukua mifupa ya Yusufu na wakaenda nazo jangwani ili wazizike kwa nchi ya ahadi. Yusufu alikuwa amewashurudisha wanawe kufanya hivyo miaka mingi iliyopita.

Mungu aliwaokoa Waisraeli kutoka Misri utumwani na kuwaongoza jangwani kwenda kwa nchi aliyowaahidi. Tutajifunza zaidi juu ya safari hiyo kwa somo lifuatalo.